**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA KUMI NA NNE

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KWANZA

**29 JANUARI, 2019**

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 29 JANUARI, 2019

### I. WIMBO WA TAIFA:

Wimbo wa Taifa uliimbwa kwa kuongozwa na *Brass Band.*

### II. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Yustino Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

### IDADI YA WABUNGE WALIOHUDHURIA:

### MAKATIBU MEZANI:

1. Ndg. Steven Kagaigai
2. Ndg. Ramadhan Abdallah
3. Ndg. Joshua Chamwela
4. Ndg. Ruth Makungu

### III. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Abdallah Ally Mtolea aliapa Kiapo cha Uaminifu.

### IV. TAARIFA YA SPIKA:

Mhe. Spika alisoma Taarifa ya Miswada iliyosainiwa na Rais kuwa Sheria kama ifuatavyo:-

1. Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Kifedha wa Mwaka 2018 *[The Microfinance Bill, 2018].*

2. Sheria ya Huduma Ndogo za Kifedha Namba 10 ya Mwaka 2018 *[The Microfinance Act, No. 10 of 2018].*

## V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Walemavu)

Aliwasilisha Mezani Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 44 la tarehe 02 Novemba, 2018;
2. Toleo Na. 45 la tarehe 09 Novemba, 2018;
3. Toleo Na. 46 la tarehe 16 Novemba, 2018;
4. Toleo Na. 47 la tarehe 23 Novemba, 2018;
5. Toleo Na. 48 la tarehe 30 Novemba, 2018;
6. Toleo Na. 49 la tarehe 07 Disemba, 2018;
7. Toleo Na. 50 la tarehe 14 Disemba, 2018;
8. Toleo Na. 51 la tarehe 21 Disemba, 2018;
9. Toleo Na. 52 la tarehe 28 Disemba, 2018;
10. Toleo Na. 01 la tarehe 04 Januari, 2019;
11. Toleo Na. 02 la tarehe 11 Januari, 2019;
12. Toleo Na. 03 la tarehe 18 Januari, 2019.

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 *[The Political Parties (Amendments) Bill, 2018].*

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:

Aliwasilisha Mezani Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 *[The Political Parties (Amendments) Bill, 2018].*

### MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA OFISI YA WAZIRI MKUU:

Aliwasilisha Mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 *[The Political Parties (Amendments) Bill, 2018].*

## VI. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na. 1: Mhe. Munira Mustapha Khatib

Nyongeza: Mhe. Munira Mustapha Khatib

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 2: Mhe. Omar Abdallah Kigoda

Nyongeza: Mhe. Omar Abdallah Kigoda

Swali Na. 3: Mhe. Gibson Blasius Ole - Meiseyeki

Nyongeza: Mhe. Gibson Blasius Ole - Meiseyeki

### WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na. 4: Mhe. Jaku Hashim Ayoub (B.L.W)

Nyongeza: Mhe. Jaku Hashim Ayoub (B.L.W)

### WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 5: Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest

Nyongeza: Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest

### WIZARA YA NISHATI:

Swali Na. 6: Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe

Nyongeza: Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe

Swali Na. 7: Mhe. Fredy Atupele Mwakibete

Nyongeza: Mhe. Fredy Atupele Mwakibete

**WIZARA YA KILIMO:**

Swali Na. 8: Mhe. Gimbi Dotto Masaba

Nyongeza: Mhe. Gimbi Dotto Masaba

Swali Na. 9: Mhe. Boniphace Mwita Getere

Nyongeza: Mhe. Boniphace Mwita Getere

Swali na. 10: Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma

Nyongeza: Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia
Mhe. Nape Moses Nnauye

**MATANGAZO:**

Wageni: Wageni mbalimbali waliokuwepo Bungeni walitambulishwa na Mhe. Spika.

Matangazo ya Kazi: Maonyesho ya Wiki ya Sheria yalitangazwa kuanza tarehe 2 Februari, 2019 na Waheshimiwa Wabunge wote walialikwa kushiriki.

## VII. HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Joakim Mhagama alitoa Hoja ya Kutengua Kanuni ya 28 (2) ili Bunge lirejee saa 10:00 jioni na Kanuni

ya 28 (15) ili Bunge lifanye kazi siku ya Jumamosi tarehe 2 Februari, 2019. Hoja iliungwa mkono na Wabunge.

## VIII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 *[The Political Parties (Amendments) Bill, 2018].*

i. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Joakim Mhagama alitoa Maelezo ya Muswada huo.

ii. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huo.

iii. Mhe. Ester Moses Bulaya, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinznai Bungeni aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huo.

Uchangiaji wa jumla ulianza na Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Joseph Kizito Mhagama | - | CCM |
| 2. Mhe. Susan Alphonce Kolimba | - | CCM |
| 3. Mhe. Halima James Mdee | - | CHADEMA |
| 4. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda | - | CCM |
| 5. Mhe. Mussa Bakari Mbarouk | - | CUF |
| 6. Mhe. Najma Murtaza Giga | - | CCM |

## IX. KUSITISHWA BUNGE:

Saa 7:00 mchana Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Naibu Spika) alisitisha Bunge hadi saa 10:00 jioni.

## X. BUNGE KUREJEA:

Saa 10:00 jioni Bunge lilirejea likiongozwa na Mhe. Job Y. Ndugai (Spika).

Mjadala juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa mwaka 2018 uliendelea na wafuatao walichangia:-

| | | |
|---|---|---|
| 7. Mhe. Zainab Athumani Katimba | - | CCM |
| 8. Mhe. Ally Saleh Ally | - | CUF |
| 9. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde | - | CCM |
| 10. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | - | CCM |
| 11. Mhe. Salome Wycliffe Makamba | - | CHADEMA |
| 12. Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe | - | ACT |
| 13. Mhe. George Boniface Simbachawenye | - | CCM |
| 14. Mhe. Saed Ahmed Kubenea | - | CHADEMA |
| 15. Mhe. William Mganga Ngeleja | - | CCM |
| 16. Mhe. Andrew John Chenge | - | CCM |
| 17. Mhe. Mohamed Omary Mchengerewa | - | CCM |

### KUHITIMISHA HOJA

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Prof. Aderladus Kabango Kilangi | - | AG |
| 2. Mhe. Jenista Joakim Mhagama | - | WN/OWM |

### KAMATI YA BUNGE ZIMA

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima kwa ajili ya kupitisha Muswada Ibara kwa Ibara. Mapendekezo yaliyowasilishwa na Mhe. Anatropia Theonest kwenye baadhi ya ibara yalikataliwa na Kamati ya Bunge Zima. Kamati ya Bunge

Zima ilipitisha Ibara zote za Muswada pamoja na Marekebisho ya Serikali.

**BUNGE KUREJEA:**

i. Baada ya Kamati kumaliza kazi yake, Bunge lilirejea na Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati na kutoa Hoja ya kuomba Bunge likubali kupitisha Muswada huo. Wabunge walihojiwa na kupitisha Muswada.

ii. Muswada uliosomwa kwa Mara ya Tatu na Spika kutangaza kwamba Muswada huo sasa umepitishwa na Bunge na hatua itakayofuata ni kusainiwa na Rais.

## XI. KUSITISHWA BUNGE:

Saa 7:45 usiku Mhe. Job Y. Ndugai (Spika) alisitisha Bunge hadi Jumatano tarehe 30 Januari, 2019 saa 10:00 jioni.